**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**
**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0757511911**
**Mkuu wa Shule 0757511911**
**Makamu Mkuu wa Shule 0657428050**
**Matron 0656377353**
**Shule ya Sekondari Mwera**
**S.L.P27. PANGANI**

**Tarehe 12/02024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWERA HALMASHAURI YA PANGANI MKOA WA TANGA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023na atasoma tahasusi ya HGL/HKL/IHG/IHK/IHL kata isiyohusika.

Shule ya Sekondari Mwera ni shule ya mchanganyiko ya kutwa kwa kidato cha I-IV na ni ya bweni ya wasichana kwa kidato cha V-VI ya michepuo ya Sanaa ikijumuisha taasusi za **HGL/HKL/IHG/IHK** na **IHL.** Shule ipo umbali wa Kilometa 11 Kusini mwa Mji wa pangani.
Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi commercial Tanga mjini Nauli ni Shilingi 5,000 mpaka kijiji cha Mwera kata ya Mwera. Utachukukua pikipiki sh. 1,000 mpaka shuleni

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ----/-----/2024 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe -----/----/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe ----/----/2024

**2.** **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule inapatikana shuleni kwa mzazi anayependa, ambapo sketi 1 na tai kwa gharama ya Tsh 20,000/=, shati la shule anunulie nyumbani ambalo ni jeupe la mikono mifupi
ii. Kwa wale waisilamu watavaa hijab short kanzu na sketi (kwa anaependa) sh. 50,000/=
iii. Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
iv. Soksi jozi mbili nyeupe
v. Sweta rangi ya daki bluu (kama utahitaji kuvaa).
vi. Nguo za michezo ni track-suit rangi ya kijivu yenye mistari myeupe pembeni (isiyombana hata kidogo), Raba za michezo nyeupe na fulana ya kijivu ya shingo ya round isiyokuwa na maandishi yoyote ( ajena nayo kutoka nyumbani )
KUMBUKA: Nguo hizi ndizo anazotakiwa kuvaa siku ya kuripoti
vii. T-shirt ya darasani itavaliwa siku ya jumatano na ijumaa tu inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 15,000/=.
viii. Nguo za kushindia (shamba dress) (zinapatikana Jirani na shuleni kwa mzazi anayependa gauni moja sh. 25,000)
Kumbuka michango tajwa hapo juu isiingizwe kwenye A/C ya shule mwanafunzi aje nayo mkononi

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

1. Ream za karatasi A4 – 3 kwa mwaka. 2 kwaajili ya matumizi ya ofisi na moja atabaki nayo kwaajili ya matumizi yake.
2. Scientific calculator 1 (fx 991) kwa wanafunzi wanaosoma jiografia.
3. Godoro futi 2 1/2 upana na urefu futi 6
4. Mashuka mawili ya rangi ya pink
5. Mto mmoja wenye foronya ya rangi ya pink
6. Nguo za ndani na taulo za kike za kutosha
7. Chandarua 1
8. Taulo ya kuogea
9. Vyombovya kulia chakula (sahani ya udongo/mfupa,bakuli ya udongo/mfupa,kikombe cha udongo na kijiko)
10. Kwanja1, jembe 1 lenye mpini, panga 1, hand broom na squeezer.

11. Ndoo ndogo 2 (moja utaikabidhi shuleni na moja ni kwa matumizi yako ya usafi)
12. Graph pad 1 kwa wanafunzi wanaosoma jeografia
13. Ndala za kuogea
14. Kamusi 1 kwa HKL na IHK ya Kiswahili kwa matumizi binafsi
15. Kamusi 1 ya kingereza kwa HGL, HKL na IHL (kwa matumizi binafsi)
16. Kwanja 1,jembe 1 lenye mpini na panga 1 kwa kila mwanafunzi
17. Reki 1 kwa HGL na IHK na ufagio 1 wa ndani (soft broom) kwa HKL, IHL na IHG.
18. Kopo 1 lenye mkono kwaajili ya matumizi binafsi
19. **Aidha mwanafunzi alipe Michango ifuatayo kwenye akaunti ya shule namba NMB 42001200031 MWERA SECONDARY SCHOOL** kisha awasirishe shuleni bank paying slip.

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3 Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

### 3.2 Heshima na utii

wanafunzi wote hawana budi kuonyesha heshima na utii mahali popote wanapokuwa shuleni na nje ya shule: I.Lugha chafu na matusi ni marufuku

II. Lazima wanafunzi kuheshimu na kuwatii viranja, walimu, wafanyakazi wasio walimu na viongozi wengine.

III. Wanafunzi hawana budi kupendana na kuheshimiana wao kwa wao.

IV. Wanafunzi ni lazima kusabahi na kusalimu watu wengine kwa kadri ya hali yao wanayostahili.
Wanafunzi wanalazimika kusimama na kusalimia kwa heshima walimu wao, wafanyakazi wasio walimu, viongozi wengine wanaoitembelea shule ikiwa ni pamoja na wakubwa wanaokutana nao mahali popote, ndani na nje ya shule. Lugha ya mawasiliano shuleni ni kiingereza tu.

V. **Ni lazima** kusimama mwalimu aingiapo darasani na kusalimia
Wanafunzi wanatakiwa kutii amri zitolewazo hapa shuleni na kuzingatia sana maagizo: i.
Sehemu zifuatazo zitatembelewa kwa ruhusa maalumu:

- Nyumba za wafanyakazi

- Hospitali, posta bank na kwenye nyumba za ibada

- Maduka ya mjini(Mwera/Pangani)

- Jengo la utawala

ii. Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika eneo la mabweni na kuingia mabwenini. Hivyo basi mwanafunzi haruhusiwi kuongea au kupiga gumzo na mtu yeyote asiyekuwa mwanajumiya wa shule hii katika eneo lolote la shule bila kibali cha mwalimu wa zamu. Kwa hiyo mwanafunzi haruhusiwi kukaribisha au kupokea mgeni wake nje ya utaratibu wa shule.

iii. Ni marufuku mwanafunzi wa shule hii kuwa na simu ya mkononi. Mawasiliano kati ya wazazi/mlezi yatafanyika kupitia ofisi ya mkuu wa shule kwa simu zilizoonyeshwa kwenye ukurasa wa kwanza. Nimarufuku mzazi kupiga simu shuleni kutaka kuongea na mtoto bila sababu ya msingi mawasiliano yatafanyika jumamosi na jumapili ya mwisho wa mwezi tu.

iv.siku ya kuwatembelea Watoto ila sio kwa ulazima ni kila jumamosi ya mwisho wa mwezi tu.

v. Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na masuala ya mapenzi, kuwa na madawa ya kulevya na vileo vingine na kuvitumia au kuviuza.

vi. Ni marufuku kwa mwanafunzi kujihusisha na tabia za usagaji/ushoga.

.

**3.2 MAHUDHURIO:**

1. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie pale anapotakiwa bila kukosa wala kuchelewa.

2. Ni lazima mwanafunzi awepo shuleni muda wote wa masomo

3. Ni lazima mwanafunzi awahi na kushiriki katika shughuli zote za shule kama kuitwa majina “Roll Call”

4. Ruhusa ya kuondoka shuleni kwa ajili ya shida nzito kama msiba itatolewa na mkuu wa shule au makamu wake iwapo atakuwa hayupo mkuu wa shule.

5. Ruhusa ya kwenda Hospitali itatolewa na matroni au muuguzi wa shule baada ya kumwona mwanafunzi mgonjwa akishirikiana na mwalimu wa zamu.

    1. Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni ndie anayeruhusiwa kumwombea mwanafunzi ruhusa kila itakapolazimika kufanya hivyo na sio vinginevyo, au kutembelea shuleni siku zilizopangwa (Jumamosi ya mwisho wa mwezi).

**3.3 UVAAJI SARE NA UNADHIFU:**

1. Vazi rasmi la shule huvaliwa wakati wote wanafunzi wakiwepo shuleni na penginepo kwa shughuli za kielimu/kishule na pia mwanafunzi aendapo au kurudi shuleni wakati wa kwenda au kutoka likizo .

2. Hereni, bangili,vipini,kofia,shanga,miwani ya jua mikufu na pete za aina yoyote **havitarusiwa** kuvaliwa shuleni.

3. Nywele: Mwanafunzi atakata nywele wakati wote. Ni marufuku kusuka,kuweka dawa au kufuga nywele ndefu au kufuga na kupaka rangi kucha

    i.

    ii. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

iii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule; iv. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation);

v. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

vi. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

vii. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

x. Kutunza mali za shule;

xi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

4 **Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kufuga ndevu;

vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

viii. Uvutaji wa sigara;

ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xi. Kusababisha mimba;

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni; xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule; xv. Kudharau Bendera ya Taifa;

xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (3) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule: J. Mziray**

**Jina la Mkuu wa Shule : Jausia Mziray**

**Mhuri wa Mkuu wa shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO AMBAPO MUDA WOTE MWANAFUNZI AWAPO SHULENI NDIZO UTAKAZO ZITUMIA NA SIVINGINEVYO**

- ➢ **Mkuu wa shule 0757511911**
- ➢ **Mwandamizi Malezi 0656377353**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA SHULE YA SEKONDARI MWERA**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

**PICHA**

A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:

JINA LA MWANAFUNZI ………………………………………………………………

TAREHE YA KUZALIWA ………………………………………………………………

MAHALI ALIPO ZALIWA (MKOA/WILAYA) ……………………………………………

MNAISHI/MNAKAA WAPI (KATA/MTAA)…………………………………………………

URAIA ……………………………………………………….

SHULE ALIYOTOKA ……………………………………………….

NAMBA YA MTIHANI ……………………………………………

B: TAARIFA YA MZAZI: JINA LA MZAZI/MLEZI …………………………………………………………………………………………………… KAZI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………………… ANUANI YA MZAZI/MLEZI ……………………………………………………………..

SIMU YA MZAZI/MLEZI: KAZINI ………………………………………………...

NYUMBANI …………………………………… MKONONI ……..………………………..

C: KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA:

Mimi ………………………………………………………… Kidato ………………… mwaka …………….. Nimesoma na nakuayaelewa yote. Kwa hiyo nakubalia kuipokea /sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimepokea maagizo au maelekezo bila kulazimishwa na nitayazingatia.

Tarehe ........................................... Saini ..................

D:KUKUBALISHERIAZASHULE:/ MWANAFUNZI.

Mimi ………………………………………………………………… Nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na naahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria za shule na maelekezo mengine nitakayo pewa na walimu wote wa shule, nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwedhidi yangu kwa kanuni, taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe ………………………………………….. Saini …………… ………………

**FOMU YA MZAZI/MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA/MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE**

E: MAZAZI/ MLEZI – (ajaze sehemu hii)

i. Mimi …………………………………………………ambaye ni Mzazi/mlezi, nathibitisha kuwa mwanangu ……………………………………………jina la (mtoto)ameelewa maagizo ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanagu ni ……………………………… dhehebu lake ni ……………………………………………

ii. Ninaruhusu/siruhusu (kata isiyohusika) mwanangu kushiriki katika makongamano au warsha za kidini nje ya shule zinazofanyika nje na ndani ya mkoa wa Tanga zitakazo fanyika kwa ruhusa ya mkuu wa shule hii.

iii. Nimeruhusu/ siruhusu (kata isiyohusika) wakati w a likizo fupi (mid term) mwanangu atoke shuleni na kwenda kwa …………………………………………………..……… wa (mahali) ………………………………………………….. uhusiano wake na mwanangu ni ………………………………….. namba yake ya simu ni ………………………………………………

iv. Aidha

mimi ……………………………….…………….. ambaye ni mzazi/mlezi,nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo mengine ya shule yanayohusu mwanafunzi (jina la mwanafunzi) ………………………………………………………naahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa mzazi/mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kumtimizia mahitaji yake ya shule.

(v) picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 8 | |

JINA LA MZAZI /MLEZI NDUGU 1 NDUGU 2

…………………………….. ………………………. ……………………….

SIMU…………………….. ………………………. ………………………. ………………

UHUSIANO…………….. ……………………….. …….. …………….. JINA LA MZAZI/MLEZI SAINI

TAREHE…………………

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

PART A THE HEADMISTRESS,

MWERA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 27,
PANGANI – TANGA.

TO,
The Medical office,
……………………………
…………………………… ……………………………
…………………………………………………….( Name of student in full) please examine the above mentioned student as to her physical and mental fitness for a full time student. The examination should include the following category (a- c)

a. (i). Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Venereal disease (v) Limbs

b. Neurosis

c. Other serious diseases eg. Asthma, Tb etc

Name ……………………………………….………… Date ……………………..signature

…………………
PART B: MEDICAL CERTIFICATE
(to be completed by a Government Medical Officer) I have examined the above student and consider that she is fit/unfit full time studies.

i. Eyesight ………………………………………………….

ii. Hearing ……………………………………………………



iii. Speech
…………………………………………………..

iv. Limbs ………………………………………………………

v. Venereal diseases …………………………………………….
vi. Leprosy
……………………………………………………….

vii. Epilepsy ……………………………………………………

viii. Neurosis ……………………………………………………

ix. Other serious diseases eg. Asthma ……………………………………..

x. T.B ……………………………………………………………….

Other Comments ……………………………………………………………………
Name ……………………………………………….. Date ………………… Signature ……………………
STATION ……………………………..………………….. DESIGNATION ……………………………..
**Official stamp**……………………………………..